



TIST HABARI MOTOMOTO JUNE 2025

www.tist.org. Email: info@tist.org Tel. +255784-537720



In this newsletter, we are going to have:

- I. Welcome Note for the new Small Groups
- II. TIST Small Groups (Formation of TIST Groups, Benefits, Training and TIST Values)

TIST HABARI MOTO MOTO

Welcome to the TIST Program!

We send greetings from all those who support the TIST program, to all members in your Small Group.

We are happy that your Small Group decided to join many other Small Groups in TIST. TIST is "The International Small Group and Tree Planting Program". It is an environmental care and sustainable development program that aims to help rural people in developing countries to improve their environment and their lives. Most of the participants are low-income farmers, i.e. they do subsistence farming living in dry land areas facing the effects of deforestation, drought and lack of adequate food. Farmers creatively find solutions to their own challenges, for environmental, economic and social problems.

TIST is a fast growing program that is working around the world. TIST Small Groups are making a difference in their environments. The Small Groups have already planted over 29.2 million trees in Kenya, Uganda, India and Tanzania!

Every week new groups just like yours gather in different countries. They cooperate and care for each other. They plan how to create nurseries, plant seedlings, prepare land for new trees, improve agriculture practices. They develop and share new ideas with other Small Groups.

We hope that your Small Group will have success and enjoy the benefits of TIST. We are eager to serve your Small Group. Tell us what information you need and what training would help your Small Group in its work and tell us how to improve the program.

This way, all participants in TIST around the world will benefit from what you learn.

Please see your Cluster Servant or TIST Coordinator if you have any questions or problems. You can also write to us through email: info@tist.org or you can send sms or whatsapp message to your Cluster Servant phone number or TIST Leader. We would be happy to hear from you!

Congratulations and welcome to TIST.

Formation of TIST Small Groups

TIST program works with small groups of 6 to 12 people who want to improve their lives and local environment by planting trees and adopting small group and sustainable agriculture Best Practices. Small Groups prepare seedlings and plant them in their local area.

Interested farmers who want to join TIST can contact TIST Coordinator or Cluster Servant. . A farmer will be required to form a Small Group of 6-12 from at least 3 families. A Cluster Servant will train you about what is TIST and Small Group Formation Your new Small Group will be required to start doing weekly meetings (at Small Group Level) and also attending Monthly Cluster Meeting.

Getting started your group you will need to:

- Create a name for the group
- Sign a GHG Contract

TIST HABARI MOTO MOTO

In order to join TIST Small Groups should agree to;

-Start doing weekly meetings and follow the TIST Values.

-Follow TIST Best Practices for their area, rainfall, and soil conditions. Small Groups usually find that the Best Practice is to plant at least 500 new trees of various food producing, indigenous, and multi-use trees per year for at least three years and replace those trees that die.

-Keep trees in the TIST grove for a minimum period of 60 years, except when implementing Best Practices. The current Best Practice is that 10 years after the trees were planted; Small Groups may responsibly thin up to 5% of live trees each year on each grove or farm plot.

Participate in Cluster meetings or TIST seminars to help develop TIST Best Practices that are beneficial to your activities

-Comply with all current local, district, and national laws and regulations that apply to the Small Group's activities and provide any reports required by those laws and regulations.

Benefits that Small Groups receive after joining TIST:

-Small Groups own the trees.

-Trees provide the Small Groups with shade, better soil, fruit, nuts, firewood, medicine, and material for crafts

-Trees help stop erosion and improve the water supply

-Each year Small Groups will receive payments from TIST for every living tree. The more live trees that groups have, the more money they will receive.

-TIST will help Small Groups get training in tree planting, nursery development, sustainable development best practices, beekeeping, business skills, saving money and other skills that can help

- TIST Small Groups tree planting will create Greenhouse Gas credits.
- Improved cooking stoves (Banifu Stoves)
TIST provides training and access to improved cooking stoves.
Improved cooking stoves use less wood and are more efficient
Improved cooking stoves are good for your health, because you inhale less smoke compared to natural stoves.
- Organic Farming
Organic Farming (CF) helps farmers get more crops in a smaller area.
Organic Agriculture helps to get crops even when there is little rain
TIST teaches to use Organic Farming methods to prepare fields by digging holes during the summer and applying natural fertilizers.
- Manure fertilizer training
TIST provides training on making manure and compost. This allows farmers to avoid buying fertilizers, get more yield, and improve and care for the environment
- Farmer's health
We value the farmer's and their families.
TIST provides training on wellness and common health issues
- To develop leadership skills/talents
Every member of TIST has a chance to be a leader. TIST provides leadership training for women, men and youth
The TIST program implements Rotational Leadership, which gives everyone the opportunity/chance to lead

Training for a new Small Group

As a TIST Small Group you will receive training in the various aspects of the TIST Program including good nursery development practices, land preparation and tree planting techniques, working effectively in small groups, identifying and sharing Best Practices, conservation farming, and managing finances, and other skills.

TIST trainers, experts and trainers from other areas of the country and the world will provide the training. Some of the training workshops will be held in central locations and other trainings will be held at the Cluster Meetings.

The entire Small Group may receive training or it may be given to representatives from each group on a rotating basis may receive the training. Those members will then go back and explain the training to the other members of their group.

Your Small Group will be guided through the Application Process and taught about Small Groups Best Practices (weekly meetings, Rotational & Servant leadership, Kujengana, Action planning, Raised Nursery Management etc.)

Each member of your Small Group should be attending a Cluster meeting every month. Your Small Group will be issued with Application Process document.

Things that each of your Small Group members need to learn and understand during Application Process.

1. Each member should learn and understand Tree species and their importance (You will be also trained on Trees that do not qualify for carbon)
2. Each member should learn and understand how to establish Tree Nurseries
3. Each member of your Small Group should be attending weekly Small Group meetings using TIST Best Practices
4. Your Small Group should start practicing Rotational and Servant Leadership and Kujengana
5. Each member should learn and understand how to practice Conservation Farming
6. Each member should learn and understand GhG Contract
7. Each member should learn and understand Small Group Eligibility Requirements

Your Cluster Servant will use pendragon form to register your Small Group as Applicant Group.

TIST HABARI MOTO MOTO

TIST Values

As TIST Family we have our Values which most of TIST Small Groups know and practice. We always reflect on these Values and to ensure that we all are truly living by them. The success of TIST is based on the integrity and effort of individual members within TIST. What we can achieve depends on each of us following these Values;

Who are we?

- (i) We are Honest
- (ii) We are Accurate
- (iii) We are Transparent
- (iv) We are Servants to each other
- (v) We are Mutually Accountable to Each Other and
- (vi) We create Low Budget/ cost, yet we achieve Big Results

How we do things that other people can see

- 1) We are committed
- 2) We do our work in small groups
- 3) We seek and use the best way
- 4) We use our minds and hands.

What do we do?

- 1) We plant different species of trees for long -term
- 2) We find ways to improve our health
- 3) We practice Conservation Farming
- 4) We do other projects and businesses (sustainable agriculture, nurseries, citrus growing, dairy goats and farming, chickens, bee keeping, fishponds and fish keeping, silkworm farming etc.)
- 5) We sell carbon credits

What do we create?

- 1) We create team work – by doing things this way; we end up working as a team.
- 2) We create capacity – we create organization, strength, and a system that is strong.
- 3) We create enjoyment – we see results, we accomplish big things that we enjoy.
- 4) We create Big Results - In Conservation Farming and from other projects and business that we do.
- 5) We Create Big Results with Low Budgets



TIST HABARI MOTOMOTO JUNI 2025

www.tist.org. Email: info@tist.org Tel. +255784-537720



Katika jarida hili, tutakuwa na:

- (I) Ujumbe wa Ukaribisho kwa Vikundi Vipya
- (II) Vikundi vya TIST (Uundaji wa vikundi, Mambo ya kufanya, Faida, Mafunzo na Maadili ya TIST)

Karibu kwenye Mradi wa TIST

Wanachama wote wa kikundi, pokeeni salamu kutoka kwa wadau wote wanaosaidia Mradi huu wa TIST.

Tunayo furaha kwa kikundi chenu kuamua kujiunga na vikundi vingine vingi katika mradi huu.

TIST ni Mpango wa kimataifa wa vikundi vidogo vidogo juu ya upandaji miti. Ni mpango wa utunzaji mazingira na maendeleo endelevu unaolenga kusaidia watu wa vijijini katika nchi zinazoendelea ili kuboresha mazingira na maisha yao. Washiriki wengi ni wakulima wenye kipato cha chini yaani wanafanya kilimo cha kujikimu wanaoishi katika maeneo ya nchi kavu, yanaokabiliwa na athari za ukataji miti, ukame na hali ya kutopata chakula cha kutosheleza. Wakulima wanawezeshwa kupata ufumbuzi wa changamoto zao wenyewe, kwa matatizo ya kimazingira, kiuchumi na kijamii.

TIST ni mradi unaokuwa haraka na unaofanya kazi ulimwengu mzima. Vikundi vinavyofanya kazi katika mradi huu wa TIST vinafanya mabadiliko katika Mazingira. Mpaka sasa Vikundi vidogo vya mradi huu vimeshapanda miti zaidi ya milioni 29.2 katika nchi za Kenya, Uganda, India na Tanzania!

Kila wiki vikundi vipya kama cha kwenu hukusanyika katika nchi mbalimbali. Wanachama wake wanasaidiana wao kwa wao. Wanapanga jinsi ya kuanzisha vitalu, kupanda miche, na kuandaa sehemu za kupanda miti na kuboresha njia bora katika mambo ya kilimo. Kuendeleza na kushirikishana Mbinu Bora mbalimbali wanazozigundua kwenye vikundi vao na kutoka katika vikundi vingine.

Tuna matumaini kuwa kikundi chenu kitaleta mafanikio na kitakuwa bora kutokana na faida zilizoko kwenye mradi wa TIST. Mnaweza kutueleza mambo ambayo mnahitaji kupatiwa mafunzo au mambo ambayo yatasaidia kikundi chenu. Pia muwe huru kueleza ni mambo gani yanaweza kuboresha mradi. Kupitia njia hii ya kushirikishana wanachama wote wa mradi huu ulimwenguni kote watanufaika na faida mtakazojifunza.

Tafadhali Muoneni Mtumishi wa Klasta au Mratibu wa mradi wa TIST endapo mtakuwa na swali lolote au tatizo. Pia unaweza kutuandikia kupitia barua pepe kwa anuani ifuatayo info@tist.org, au tuma ujumbe wa kawaida au whatsapp kwa simu ya Mtumishi wako wa Klasta au kiongozi wa TIST. Tutaforahi sana kupata maoni au jambo lolote kutoka kwenu!

Hongera na karibu kwenye Mradi wa TIST

Uundaji wa Vikundi Vidogo vya TIST

TIST inashirikiana na kufanya kazi na vikundi vidogo vidogo vyenye watu kati ya 6 mpaka 12, wenye nia ya kuboresha mazingira yao na kuongeza kipato kwa kupanda miti. Hivi vikundi vinatayarisha miche ya miti na kupanda katika maeneo yao. Mkulima anayetaka kujiunga na TIST atawasiliana na Mtumishi yeyote wa TIST. Mkulima atahitajika kuunda Kikundi Kidogo kuanzia watu 6-12 walio majirani. Mtumishi wa TIST atawafundisha kuhusu TIST na Uundaji wa Kikundi Kidogo. Kikundi chako kipya kitahitajika kuanza kufanya mikutano ya kila wiki (katika Ngazi ya Vikundi Vidogo) na pia kuhudhuria Mikutano ya Klasta Kila Mwezi.

Kikundi chenu kitafuata muongozo kupitia mchakato wa Maombi na kufundishwa kuhusu Mbinu Bora za Vikundi Vidogo (mikutano ya kila wiki, Uongozi wa Mzunguko na Utumishi, Kujengana, kupanga mipango kazi, Usimamizi wa vitalu vya miti n.k.

Mambo ya kuzingatia baada ya kuanzisha kikundi:

- Kutafuta jina la kikundi
- Kusoma na kusaini mkataba wa GHG

Mambo ambayo kikundi kinapaswa kufanya ili kujiunga na mradi

Mnatakiwa kuanza kufanya mikutano ya kila wiki, na kufuata Maadili ya TIST.

- Kufuata Mbinu Bora za TIST kwa eneo lao, mvua na hali ya udongo. Vikundi Vidogo kwa kawaida huona kwamba mbinu bora zaidi ni kupanda angalau miti 500 ya aina mbalimbali inayozalisha chakula (matunda), ya asili na yenye matumizi mbalimbali kwa mwaka kwa angalau miaka 3 na kufidia miti inayokufa.

-Kuacha miti kwenye shamba la TIST kwa muda usiopungua miaka 60, isipokuwa wakati wa kutekeleza Mbinu Bora. Mbinu Bora ya sasa ni kwamba miaka 10 baada ya miti kupandwa, Vikundi Vidogo vinaweza kuvuna hadi 5% ya miti hai inayopandwa kila mwaka kwenye kila shamba la miti.

-Kushiriki kwenye mikutano ya Klasta au semina za TIST kusaidia kuzalisha mbinu bora

-Kuzingatia sheria na kanuni zote za sasa za mitaa, wilaya, na kitaifa zinazotumika kusimamia shughuli za Kikundi Kidogo na kutoa taarifa zozote zinazohitajika na sheria na kanuni hizo.

-Kusaidia kuhesabu miti.

-Kutayarisha miche zaidi na kupanda miti mingi zaidi kila mwaka

Faida ambazo Vikundi vitapata vitakapojiunga na TIST

-Kikundi kitamiliki hiyo miti

-Miti itawapatia wanavikundi, vivuli, kuni, mbao, kurutubisha udongo, matunda, mbegu za mafuta – mfano korosho, dawa, malighafi za kutengenezea vinyago, vinu n.k.

-Kikundi kitapata malipo kwa kila mti ulio hai, kila mwaka, kadiri kikundi kitakavyokuwa na ongezeko la miti ndivyo kipato chao kitaongezeka

-TIST itasaidia kutoa mafunzo mbalimbali ya utengenezaji wa vitalu vya miti, upandaji na utunzaji wa miti, utunzaji wa fedha, na mambo mengine yanayoweza kuwasaidia wanavikundi katika vijiji vyao.

-TIST itavisaidia vikundi kuuza hewa ya Kaboni “Greenhouse gas credit”.

-Majiko ya kupikia yaliyoboreshwa (Majiko Banifu)

TIST hutoa mafunzo na upatikanaji wa majiko yaliyoboreshwa ya kupikia.

Majiko ya kupikia yaliyoboreshwa yanatumia kuni kidogo na yanafaa zaidi

Majiko ya kupikia yaliyoboreshwa yanafaa kwa afya yako, kwa sababu unavuta kiwango kidogo cha moshi ukilinganisha na majiko ya asili.

-Kilimo Hai

Kilimo Hai (CF) husaidia wakulima kupata mazao mengi zaidi katika eneo dogo.

Kilimo Hai husaidia kupata mazao hata mvua zikiwa chache. TIST inafundisha kutumia mbinu za Kilimo Hai ya kuandaa mashamba kwa kuchima mashimo wakati wa kiangazi na kuweka mbolea ya asili.

-Mafunzo ya mbolea ya samadi

TIST inatoa mafunzo ya kutengeneza samadi na mboji. Hii inaruhusu wakulima kuepuka kununua mbolea, kupata mavuno zaidi, pia mbinu hii huboresha na kutunza mazingira

TIST HABARI MOTO MOTO

Afya ya mkulima

Afya ya mkulima ndiyo rasilimali yetu kubwa. TIST hutoa mafunzo juu ya kuwa na afya njema na masuala ya kawaida ya kiafya

-Kuibua vipawa vya Uongozi

Kila mshiriki wa TIST ana nafasi ya kuwa kiongozi. TIST inatoa mafunzo ya uongozi kwa wanawake, wanaume na vijana.

Mpango wa TIST unatekeleza Uongozi wa Mzunguko, ambao unampa kila mtu fursa/nafasi ya kuongoza

Mafunzo kwa Kikundi Kidogo Kipya

Kama kikundi cha TIST mtapatiwa mafunzo yatakayo wawezesha kuelewa mambo mbalimbali kuhusu TIST. katika mafunzo hayo mtapata elimu juu ya utunzaji na uendelezaji wa kitalu cha mbegu, kutayarisha udogo, mbinu za upandikizaji zinavyotakiwa ndani ya kikundi, kutambua na kuchangia njia Bora, utunzaji na uhifadhi wa fedha, matumizi ya teknolojia, mbinu za hifadhi katika kilimo, na masuala mengine mengi.

Mafunzo yatatolewa na watumishi wa TIST wa eneo lako au waratibu wa TIST kutoka eneo jingine. Baadhi ya shughuli za mafunzo zitatolewa katika kituo maalumu na mafunzo mengine yatatolewa huko huko vijijini. Mafunzo yatatolewa kwa wanavikundi au kwa wawakilishi kutoka ndani ya kikundi kwa utaratibu wa kupokezana mmoja baada ya mwingine. Mtakuwa mkijulishwa juu ya taratibu na tarehe za mafunzo kwa njia ya simu, magazeti/jarida au moja kwa moja na Mtumishi wa Klasta.

Kikundi chenu kitafuata muongozo kupitia mchakato wa Maombi na kufundishwa kuhusu Mbinu Bora za Vikundi Vidogo (mikutano ya kila wiki, Uongozi wa Mzunguko na Utumishi, Kujengana, kupanga mipango kazi, Usimamizi wa vitalu vya miti, nk,

Kila mwanachama wa Kikundi chenu Kidogo anapaswa kuhudhuria mkutano wa Klasta kila mwezi. Kikundi chenu Kidogo kitapewa hati ya Mchakato wa Maombi.

Mambo ambayo kila mwanachama wa Kikundi chenu Kidogo anahitaji kujifunza na kuelewa wakati wa Mchakato wa Maombi.

1. Kila mwanachama anapaswa kujifunza na kuelewa aina za Miti na umuhimu wake. Mtaelekezwa miti inayostawi katika mkoa au wilaya yenu. (Mtafundishwa pia kuhusu Miti ambayo haina sifa kwenye biashara ya kaboni)

2. Kila mwanachama ajifunze na kuelewa jinsi ya kuanzisha Vitalu vya Miti

3. Kila mwanachama wa Kikundi Kidogo anapaswa kuhudhuria mikutano ya Kila Wiki ya Kikundi Kidogo kwa kutumia Mbinu Bora za TIST

4. Kikundi chenu Kidogo kianze kufanya Uongozi wa Mzunguko, Utumishi na Kujengana

5. Kila mwanachama ajifunze na kuelewa jinsi ya kufanya Kilimo Hifadhi

6. Kila mwanachama anapaswa kujifunza na kuelewa Mkataba wa GhG

7. Kila mwanachama anapaswa kujifunza na kuelewa Mahitaji ya Kustahiki kwa Kikundi Kidogo

Mtumishi wa Klasta atatumia fomu ya pendragon kusajili Kikundi chenu Kidogo kama Kikundi cha Waombaji.

TIST HABARI MOTO MOTO

MAADILI YA TIST

Kama Familia ya TIST tuna Maadili yetu ambayo wengi wa Wanavikundi Vidogo vya TIST wanayajua na kuyatekeleza. Daima tunatafakari juu ya Maadili haya na kuhakikisha kwamba sote tunaishi kulingana nayo. Mafanikio ya TIST yanatokana na uadilifu na juhudi za wanachama binafsi ndani ya TIST. Tunachoweza kufikia inategemea kila mmoja wetu kufuata Maadili haya;

Sisi ni Nani?

- 1) Sisi ni waaminifu.
- 2) Sisi tunatoa taarifa sahihi.
- 3) Sisi ni wawazi
- 4) Sisi tunatumikiana.
- 5) Sisi ni wawajibikaji
- 6) Bajeti Ndogo, Matokeo Makubwa

Jinsi tunavyofanya mambo ambayo watu wengine wanaweza kuona

- 1) Sisi tunajitolea.
- 2) Tunafanya kazi zetu katika vikundi vidogovidogo
- 3) Tunatafuta na kutumia njia bora
- 4) Tunatumia akili na mikono yetu.

Tunachofanya

- 1) Tunapanda aina mbalimbali za miti itakayodumu kwa muda mrefu.
- 2) Tunafanya mambo kuboresha afya zetu.
- 3) Tunafanya Kilimo Hai.
- 4) Tunafanya miradi na biashara zingine.
- 5) Tunafanya biashara ya hewa ya kaboni.

Tunafanya.

- 1) Tunaunda kazi ya timu—kwa kufanya mambo kwa njia hii; tunaishia kufanya kazi kama timu.
- 2) Tunajenga Uwezo-tunaunda shirika, nguvu, na mfumo ambao ni imara.
- 3) Tunafanya mambo yanayotufurahisha-tunaona matokeo, tunatimiza mambo makubwa ambayo tunafurahia
- 4) Tunafanya mambo yanayoleta matokeo makubwa-matokeo makubwa ya upandaji miti. matokeo makubwa katika Kilimo Hai na matokeo makubwa kutokana na miradi na biashara zingine tunazofanya.
- 5) Tunapata matokeo makubwa kwa kutumia gharama ndogo